# JIMBO KATOLIKI LA GEITA

### HOSPITALI TEULE YA HALMASHAURI YA WILAYA YA SENGEREMA

**Unapojibu tafadhali taja**
**Kumb. Na. SCDH/GCL/VOL. II/35/2021** **28/07/2022**

## TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI:

Hospitali Teule Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema inaendeshwa chini ya Jimbo Katoliki la Geita ikishirikiana na Serikali Wizara ya Afya chini ya Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri Wilaya ya Sengerema katika utoaji wa huduma za afya kwa wananchi.

Aidha Katika ushirikiano huo, hospitali imepata kibali cha **AJIRA MPYA** trarehe 25/07/2022 kutoka kwa **Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais Menejiment ya Utumishi wa Umma na Utawala bora** chenye **Kumb. Na. FA. 10/128/01/"K"/104** ya tarehe 09/06/2022.

Mganga Mfawidhi wa Hospitali Teule Halmashauri ya wilaya ya Sengerema anapenda kutangaza nafasi sita za ajira kwa kada mbalimbali za afya kama ifuatavyo;

1. Daktari daraja la II — Nafasi 1
2. Daktari Msaidizi wa Meno — Nafasi 1
3. Tabibu daraja la II — Nafasi 2
4. Afisa Mtekonolojia — Nafasi 1
5. Afisa Muuguzi Msaidizi daraja II — Nafasi 1

**SIFA ZA JUMLA KWA WAOMBAJI**

i. Mwombaji anatakiwa awe Raia wa Tanzania na wenye umri usiozidi miaka 45.
ii. Mwombaji aambatishe cheti cha kuzaliwa
iii. Mwombaji ambaye tayari ni Mtumishi wa Umma na amejipatia sifa za kuingilia katika kada tofauti na alizonazo, apitishe barua yake ya maombi ya nafasi za kazi kwa Waajiri wake.
iv. Mwombaji aambatishe maelezo binafsi yanayojitosheleza (Detailed C.V) yenye anwani na namba za simu zinazopatikana pamoja na majina ya Wadhamini (referees) watatu wa kuaminika.

v. Maombi yote yaambatishwe na vyeti vya taaluma, maelezo, nakala za vyeti vya Kidato cha nne na kidato cha sita kwa wale waliofikia kiwango hicho na vyeti vya kuhitimu mafunzo mbalimbali kwa kuzingatia sifa za kazi husika.
   - ✓ Certificates
   - ✓ Cheti cha mtihani wa Kidato cha IV na VI
   - ✓ Computer Certificate
   - ✓ Vyeti vya kitaaluma (Professional certificate from respective boards)
   - ✓ Picha moja "Passport size" ya hivi karibuni.

vi. Testmonial":, **"Provisional Results", "Statement of Results", hati matokeo za kidato cha nne na sita (FORM IV AND FORM VI RESULTS SLIPS) *HAVITAKUBALIWA***

vii. Mwombaji aliyesoma nje ya Tanzania ahakikishe vyeti vyake vimehakikiwa na kuidhinishwa na Mamlaka husika (TCU au NECTA).

viii. Mwombaji wa nafasi ya Ajira aliyestaafishwa/kuachishwa kazi katika Utumishi wa Umma haruhusiwi kuomba isipokuwa kama anakibali cha Katibu Mkuu Kiongozi.

ix. Mwombaji wa kazi ambaye tayari ni mwajiriwa katika nafasi ya kuingilia aliyeko katika Utumishi wa Umma asiombe kwa kuzingati maelekezo yaliyo katika **Waraka Na. CAC. 45/257/01/D/140** wa tarehe **30 Novemba ,2010**.

1. ***Uwasilishaji wa taarifa na sifa za kughushi wahusika watachuliwa hatua za sheria.***

*1.* **DAKTARI DARAJA LA II Nafasi 1**

**SIFA ZA MUOMBAJI:**

- Awe na cheti na kufaulu kidato cha nne au kidato cha sita.
- Mwenye shahada ya Udaktari wa binadamu katika chuo kikuu kinachotambuliwa na serikali.
- Awe kamaliza mafunzo kwa vitendo 'internship' kwa muda usiopunguwa mwaka mmoja.
- Awe kasajiliwa na kupata cheti cha usajili kutoka baraza la madaktari Tanganyika. ' Medical Council of Tanganyika
- Kuwa na leseni ya baraza la kitaaluma ambayo haijaisha muda wake.

Kiwango cha mshahara ni kulingana na muundo wa maendeleo ya utumishi kwa kada zilizo chini ya wizara ya afya wa mwaka 2009 Nyongeza II : Muundo wa Utumishi wa Madaktari wa binadamu.
Utazingatia ngazi ya Mshahara wa Serikali TGHS E1 kwa mwezi.

**KAZI NA MAJUKUMU :**

i. Kufanya kazi zote za matibabu hospitalini zinazohusiana na magonjwa mbalimbali yakiwemo magonjwa ya Watoto, magonjwa ya kinamama na upasuaji wa kawaida na dharura.

ii. Kutoa na kusimamia elimu ya afya pamoja na kuboresha afya ya jamii katika wilaya na mkoa nae neo lake la kazi.

iii. Kuchunguza, kufuatilia na kuzuia milipuko ya magonjwa.

iv. Kutunza takwimu na kuzitumia kama inavyoelekezwa katika misingi ya MTUHA.

v. Kupanga na kutathimini huduma za afyaika eneo lake la kazi.

vi. Kufundisha wanafunzi na watumishi waliopo kwenye eneo lakazi.

vii. Kusimamia na kuelekeza wafanyakazi walio chini yake.

viii. Kufundisha wanafunzi katika vyuo vya afya vilivyopo eneo lake la kazi.

ix. Kubuni na kuendesha utafiti na kusambaza matokeo.

x. Kubuni na kutayarisha mikakati ya kuinua ubora wa huduma ya fani yake.

xi. Kuandaa mipango na makisio ya bajeti ya huduma za afya.

xii. Kushuriki, kuhakiki na kuboresha huduma za afya (medical audit and quality improvement).

xiii. Kutoa huduma za mkoba (outreach) katika wilaya/mkoa wake

xiv. Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na mkuu wake wa kazi zinazohusiana na elimu, uzoefu na ujuzi wake.

**2. DAKTARI MSAIDIZI WA MENO DARAJA LA II Nafasi 1**

**SIFA ZA MUOMBAJI:**

- Awe na cheti na kufaulu kidato cha nne au kidato cha sita.
- Mwenye stashahada ya juu ya tiba ya meno katika chuo kinachotambuliwa na serikali.
- Awe kasajiliwa na kupata cheti cha usajili kutoka baraza la madaktari Tanganyika. ' Medical Council of Tanganyika.
- Kuwa na leseni ya baraza la kitaaluma ambayo haijaisha muda wake

Kiwango cha mshahara ni kulingana na muundo wa maendeleo ya utumishi kwa kada zilizo chini ya wizara ya afya wa mwaka 2009 Nyongeza V : Muundo wa Utumishi wa Madaktari. Utazingatia ngazi ya Mshahara wa Serikali TGHS C1 kwa mwezi.

**KAZI NA MAJUKUMU :**

i. Kutoa elimu ya afya ya kinywa na meno kwenye miradi ya (Primary Health Care) PHC akishirikiana na waratibu wa PHC

ii. Kuweka kumbukumbu sahihi na kufanya makisio ya kuendesha shughuli za afya ya kinywa na meno

iii. Kupanga na kutekeleza mpango wa masomo ya kujiendeleza kazini

iv. Kutoa huduma ya kwanza kwa matatizo yatokanayo na ajali

v. Kutibu magonjwa ya kinywa na meno.

vi. Kufanya kazi za rufaa zitakazoelekezwa kwake na walio chini yake

vii. Kazi zingine atakazopangiwa na mkuu wake wa kazi.

3. **TABIBU DARAJA LA II Nafasi 2**

- Awe na cheti na kufaulu kidato cha nne au kidato cha sita.
- Mwenye stashaha ya tabibu ya muda wa miaka mitatu katika chuo kinachotambuliwa na serikali.
- Awe kasajiliwa na kupata cheti cha usajili kutoka baraza la madaktari Tanganyika. ' Medical Council of Tanganyika na leseni ya baraza la kitaaluma.

Kiwango cha mshahara ni kulingana na muundo wa maendeleo ya utumishi kwa kada zilizo chini ya wizara ya afya wa mwaka 2009 Nyongeza VI : Muundo wa Utumishi wa Tabibu.

Utazingatia ngazi ya Mshahara wa Serikali TGHS B1 kwa mwezi.

**KAZI NA MAJUKUMU**

i. Kazi zote zinazofanywa na tabibu msaidizi.
ii. Kutambuwa na kutibu magonjwa ya kawaida.
iii. Kusimamia utendaji wa watumishi walio chini yake na kufanya upasuaji mdogo.
iv. Kushiriki katika kupanga na kutekeleza huduma za afya msingi.
v. Kushauri na kuhamasisha wananchi kuchangia huduma za afya za mfuko wa afya ya jamii.
vi. Kuweka kumbukumbu za vifaa na zana za kutolea huduma.
vii. Kuweka kumbukumbu, kuandaa na kutoa taarifa za utekelezaji
viii. Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na mkuu wake wa kazi.

4. **AFISA MTEKINOLOJIA DARAJA LA II Nafasi 1**

- Awe na cheti na kufaulu kidato cha nne au kidato cha sita.
- Mwenye shahada ya sayansi ya maabara ya binadamu kutoka katika chuo kikuu kinachotambuliwa na serikali na kusajiliwa na mabaraza ya taaluma.
- Kuwa na leseni ya baraza la kitaaluma ambayo haijaisha muda wake

Kiwango cha mshahara ni kulingana na muundo wa maendeleo ya utumishi kwa kada zilizo chini ya wizara ya afya wa mwaka 2009 Nyongeza XI : Muundo wa Utumishi wa Maafisa Mtekonoloji.
Utazingatia ngazi ya Mshahara wa Serikali TGHS C1 kwa mwezi.

**KAZI NA MAJUKUMU**

i. Kufanya uchunguzi wa kimaabara (haemotology/parastology, microbiology, immunology, blood groop serology, entomology clinical chemistry and hostopathology) katika maabara za afya na utafiti (Research laboratories)
ii. Kufundisha wanafunzi katika taasisi mbalimbali za afya, masomo yanayoendana na taaluma ya maabara.
iii. Kuchukuwa sampuli zinazohitaji utaalamu maalum na sampuli kwa ajili ya uchunguzi katoka maabara nyingine za afya na utafiti.
iv. Kuweka kumbukumbu za matokeo ya vipimo katoka rejista
v. Ktunza vifaa na vitendea kazi vya maabara.
vi. Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na mkuu wake wa kazi zinazohusiana na elimu, uzoefu na ujuzi wake.

*5.* **AFISA MUUGUZI MSAIDIZI DARAJA LA II** **Nafasi 1**

- Awe na cheti naa kufaulu kidato cha nne au kidato cha sita.
- Mwenye stashahada (Diploma) ya uuguzi kwa muda usiopunguwa miaka miwili kutoka katika chuo kinachotambuliwa na serikali na kusajiliwa na mabaraza la wauguzi na wakunga Tanzania.
- Kuwa na leseni ya baraza la kitaaluma ambayo haijaisha muda wake

Kiwango cha mshahara ni kulingana na muundo wa maendeleo ya utumishi kwa kada zilizo chini ya wizara ya afya wa mwaka 2009 Nyongeza IX : Muundo wa Utumishi wa Maafisa wauguzi wasaidi.
Utazingatia ngazi ya Mshahara wa Serikali TGHS B1 kwa mwezi

**KAZI NA MAJUKUMU**

i. Kutoa huduma za uuguzi.
ii. Kukusanya takwimu muhumu za afya
iii. Kuwaelekeza kazi wauguzi walio chini yake
iv. Kuelimisha wagonjwa na jamii kuhusu matatizo yao ya kiafya
v. Kutoa huduma za king ana uzazi
vi. Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na mkuu wake wa kazi zinazohusiana na elimu, uzoefu na ujuzi wake.

**MWISHO WA KUTUMA MAOMBI ;**

i. Mwisho wa kupokea maombi ya kazi ni tarehe 09 **Agosti, 2022** saa **9.30** Alasiri..
ii. Maombi yatakayowasilishwa nje ya utaratibu uliobainishwa katika tangazo hili **HAYATAFIKIRIWA.**

**JINSI YA KUTUMA MAOMBI ;**

Maombi yote yatumwe kwa njia ya **Posta** kupitia anuani ifuatayo;

Mganga Mfawidhi,
Sengerema hospitali
S.L.P 20, Sengerema Mwanza

**TANGAZO HILI LIMETOLEWA NA;**

**MGANGA MFAWIDHI**
**SENGEREMA HOSPITALI**

**SENSA KWA MAENDELEO, JIANDAE KUHESABIWA**